AckySHINE.com

# Ndoa ya kulazimishwa

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndoa ya kulazimishwa ni ile ambayo mwanamume au mwanamke anaozwa bila yeye mwenyewe kukubali kufunga ndoa kwa hiari yake. Katika mazingira hayo wasichana au wavulana wanalazimishwa kufunga ndoa. Wakati mwingine wazazi wanafikiri wanajua nini kizuri kwa watoto waona hivyo kuwachagulia mume au mke.

Mara nyingi wazazi wanafikiria mambo ya uchumi na kijamii katika kumchagulia msichana au mvulana nani amwoe. Wanaweza kujaribu kumwoza mtoto wao katika familia ya kitajiri. Sababu nyingine inayolazimisha mtu kuoa ni mimba. Iwapo binti, amepata mimba yeye na mvulana aliyempa mimba wanalazimishwa kufunga ndoa kwa sababu baadhi ya jamii hazikubali watoto wa nje ya ndoa. Mara nyingine vijana wanalazimishwa kuoa kwa sababu wamefikia umri ambao jamii inawategemea kuoa. Mara nyingi kuna utii wa amri ya kuoa kwa vile mvulana au msichana anaogopa kutengwa na kufukuzwa na mara nyingine anatishiwa, mateso na unyanyasaji wa kimwili.